JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA NANE

26 JUNI, 2026

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA NANE – TAREHE 26 JUNI, 2026

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

687. MHESHIMIWA YOHANA STEPHEN MSITA (ITIGI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itamalizia ujenzi wa Maboma ya Zahanati katika Jimbo la Itigi.

688. MHESHIMIWA MARY DANIEL SURATI (SERENGETI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha huduma za afya kwa Wananchi wanaoathiriwa na Wanyamapori Serengeti.

689. MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti wimbi kubwa la Watumishi wa Afya na Elimu kuhama toka Vijijini kwenda Mijini baada ya kuajiriwa.

690. MHESHIMIWA SHEILA EDWARD LUKUBA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Shule mpya au kuongeza madarasa katika Shule ya Msingi Kilongo – Kihonda kutokana na ongezeko kubwa la Wanafunzi.

691. MHESHIMIWA YAHYA ALLY MHATA (NANYUMBU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Shule nne mpya za Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

692. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (IRAMBA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mkalama.

WIZARA YA UJENZI:

693. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Mkandarasi aliyeshinda Kandarasi ya ujenzi wa Barabara ya Sengerema hadi Nyehunge atapewa malipo ya awali ili aanze kazi.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

694. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itatatua migogoro ya ardhi katika maeneo ya Korotambe na Remagwe, Marasibora - Rorya na Nyamerambaro - Tarime.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

695. MHESHIMIWA MABULA JOHNSON MAGANGILA (MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kukutana na Wazazi wa Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ikiwemo yatima na wenye Ulemavu.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

696. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza ajira kwa Vijana na Wanawake katika Sekta ya Utalii.

III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

(a) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa Mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 02) Bill, 2026];*

(b) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 *[The Agricultural (Amendments) Bill, 2026];* na

(c) Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026.

IV. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:

V. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:

WAZIRI MKUU:

VI. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA AFRIKA MASHARIKI:

DODOMA
26 JUNI, 2026

BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE